**Maswali na Majibu**

1. Nani alikuwa kiongozi mpya baada ya Musa?
   *Yoshua ndiye alikuwa kiongozi mpya.*
2. Mungu alisema lazima Waisraeli wafanye nini baada ya kuingia kwa nchi?
   *Lazima waue watu wa huko wote na kuharibu sanamu zao.*
3. Nani aliwaokoa Wapelelezi kule Yeriko? *Rahabu aliwaokoa.*
4. Wapelelezi waliahidi Rahabu nini?
   *Walimwaahidi kwamba wataokoa Rahabu na familia yake.*
5. Waisraeli walivuka Mto wa Yordani uliofurika namna gani?
   *Mungu alifanya mto ukaacha kuteremka. Makuhani walisimama katikati ya mto na watu wakavuka nchi Kavu.*
6. Mungu aliambia Waisraeli lazima wangefanya nini ili waichukue Yeriko?
   *Watembee wakizunguka ukuta mara moja kwa siku 6 na mara 7 kwa siku ya 7 na makuhani wapige Tarumbeta, watu wakipiga kelele na kuta zianguke chini.*
7. Yoshua aligawanya kila kabila ya Israeli namna gani?
   *Mungu alionyesha Yoshua vile watagawana.*
8. Nani alipea kila familia pahali pake? Mbona lazima <u>wasiuze?</u>
   *Mungu aliwapa hiyo nchi. Ilikuwa ya familia yao milele*.
9. Walawi waliishi wapi? *Katika miji ya nchi ya kila kabila*.
10. Mbona walawi waliishi kwa kila kabila?
    *Ili wafunze watu wote maneno ya Mungu na sheria zake.*

## Mistari ya kukariri

Yoshua 1:6 Waebrania 11:31

## Mazungumzo

Mungu aliambia Waisraeli wajitenge na watu wa hio nchi waliokuwa wakiabudu sanamu. Zungumza vile tunaweza kujitenga na watu wasiotii Mungu na watutoe kwa njia za Mungu.

## Kuandika

Andika vile Waisraeli walipata Yeriko

# Masomo ya watoto wakubwa wa CBM

## Somo la 17 Waisraeli wanaingia kwa Nchi ya Ahadi

**SOMA Yoshua 1:5 – 6; Yoshua 2; Yoshua 3:14 – 17**

**SOMO**

Baada ya miaka 40 jangwani, watu walikuwa waende kwa nchi yenye Mungu aliwaahidi. Musa alikuwa mzee. Alikuwa na miaka 120. Mungu alikuwa amesema kwamba Musa hataenda kwa hiyo nchi. Musa aliwabariki watu wote. Halafu alipanda Mlima wa Nebo. Kule juu aliweza kuona Nchi ya Ahadi yote. Kule alikufa na Mungu akamzika. Watu waliomboleza kwa siku 30.

Mungu alichagua Yoshua kuwa kiongozi mpya. Yoshua alikuwa kiongozi mzuri sana. Alikuwa na kazi ngumu ya kufanya sasa. Alikuwa aongoze Waisraeli wapate Nchi ya Ahadi. Kulikuwa na miji ya nguvu na majitu kwa hiyo nchi. Mungu aliambia Yoshua ajibe moyo na awe mjasiri. Mungu alimwaahidi Yoshua kwamba atamsaidia.

Mungu alikuwa amesema kwamba, lazima waondoe na waharibu kabila zote zenye zilikaa kwa hiyo nchi. Lazima waharibu hao watu na sanamu zao. Lazima wasioe watu wowote wa kule.

Hili lilikua jambo la maana sana. Mungu alikuwa amechagua Waisraeli kuwa watu wake wa kipekee. Aliwambia wajitenge na watu walioabudu miungu. Aliwapa sheria ili wawe mfano mzuri kwa watu walioishi karibu nao. Mtu yeyote aliyetaka kuabudu Mungu, ilimbidi kwanza awe Mwisraeli na atimize amri za Mungu, halafu ashiriki kwa ahadi za Mungu.

Yoshua aliamua kukabiliana na mji wa Yeriko. Yeriko ulikuwa ndio mji mkubwa kwa barabara kuu ya kwenda nchi ya Kanaani. Wakishinda mji wa Yeriko, wataweza kushinda na kuingia kwa urahisi.



Yeriko ulikuwa ni mji wa nguvu sana na kuta na milingo za nguvu mno. Yoshua alituma wapelelezi wawili kwenda na kuchunguza ule mji wa Yeriko.

Wale wapelelezi walienda kwa nyumba ya Rahabu. Mfalme wa Yeriko alisikia kwamba wapelelezi wako kwa nyumba ya Rahabu. Alituma askari waende wawakamate wale wapelelezi. Rahabu aliwaficha wapelelezi chini ya kitani (mimea) yenye ilikuwa inakauka juu ya dari ya nyumba yake. Rahabu aliambia wale askari uongo. Aliwambia kwamba wapelelezi walikuwa wametoka mjini. Askari walienda haraka kuwatafuta wapelelezi.

Rahabu aliambia wapelelezi kwamba watu wote wa nchi wanaogopa Waisraeli kwa sababu Mungu wao ni wa nguvu sana. Rahabu alikuwa na imani kwa Mungu. Aliuliza wapelelezi wamwokoe wakati watachukua Yeriko. Wapelelezi waliahidi Rahabu kwamba watamwokoa yeye na familia yake. Rahabu alinin'ginisha kamba nyekundu kwa dirisha lake iwe ishara kwa wapelelezi.



Nyumba ya Rahabu ilijengwa kwa ukuta wa mji. Rahabu aliwateremshia wapelelezi kwa dirisha na wakatoroka. Waliteremka ukutani kwa kutumia kamba. Walirudi kwa Yoshua salama. Waisraeli walikuwa na nguvu waliposikia kwamba watu wa hiyo nchi wanawaogopa. Waliamini kwamba Mungu atawasaidia kushinda.

Kwanza Waisraeli walitakiwa wavuke Mto wa Yordani ili wafika kwa Nchi ya Ahadi. Mto wa Yordani ulikuwa umefurika kwa hivyo ilikuwa vigumu kuvuka. Yoshua aliomba Mungu na Mungu alimwambia cha kufanya.

Makuhani walibeba Sanduku la Mungu. Watu wote walifuata nyuma. Makuhani walipokanyaga kwa mtoni, maji yaliacha kwenda. Kulikuwa na njia kavu katikati ya mto. Makuhani na Sanduku walisimama katikati ya mto hali watu walivuka n'gambo. Watu wote walipofika n'gambo, makuhani nao walivuka. Mto ulianza kuteremka.



Hatimae, Waisraeli walifika kwa nchi yenye Mungu aliwaahidi - nchi yenye Mungu alikuwa ameahidi Ibrahimu, Isaka na Yakobo.

Mungu aliwaeleza vile wanaweza kukabiliana na Yeriko. Kila siku kwa siku sita, Waisraeli wote walizunguka mji wa Yeriko mara moja. Makuhani walienda mbele na wamebeba Sanduku la Mungu. Makuhani saba walipiga tarumbeta iliyotengenezwa kutoka kwa pembe za kondoo waume. Watu wote walifuata. Walitembea wakiwa kimya.

Siku ya saba, Mungu aliambia Waisraeli wazunguke huo mji mara saba. Halafu makuhani walipiga tarumbeta kwa sauti kuu na watu wote wakapaza sauti zao. Mungu alifanya kuta za mji wa Yeriko kuanguka chini. Waisraeli waliuchoma mji. Wapelezi waliona kamba nyekundi kwa dirisha la Rahabu. Waliokoa Rahabu na familia yake kwa sababu Rahabu alikuwa na imani kwa Mungu tena aliwaokoa.

Yoshua aliwaongoza Waisraeli kushinda mji mkubwa na watu wa huko. Walishinda na kuitawala hiyo nchi.

Mungu alionyesha mahali penye kila kabila ilitakiwa kupata na kuishi. Kila kabila ilipewa mahali pake. Ilikuwa zamu ya kila kabila imalishishe kupigani na watu waliobaki mahali pao. Waliishi kule na wakafanya ukulima. Kila kabila ilipewa pahali pake na Mungu; hawakukubaliwa kuiuza. Nchi hiyo ilikuwa yao na familia zao milele.

Kabila ya Lawi hawakupewa sehemu yoyote kwa nchi. Walawi walikuwa makuhani wa Mungu. Mungu aliwapa miji ya kuishi. Aliwapa miji kutoka kwa kila kabila. Walawi waliishi kwa kila kabila ili wawafundishe juu ya Mungu na sheria zake.

